Mtandao wa Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Usawa katika Afya (EQUINET)



# Kurudisha Hali ya Afya: Kuendeleza Afya ya Watu; Kupambana na uonevu

MKUTANO WA TATU WA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU USAWA KATIKA AFYA

## MAAZIMIO

### Kwa kuzingatia:

- Mkutano wa Kasane kuhusu Usawa katika Afya wa 1997 ulithibitisha nia thabiti ya usawa katika afya kwa ngazi zote katika nchi za Kusini mwa Afrika; Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu Afya wa 1999, Azimio la Maseru kuhusu VVU na UKIMWI la 2003 na maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za SADC kuhusu uhakika wa Chakula uliofanyika Tanzania 2004;
- Kuundwa kwa EQUINET na kazi yetu tangu 1998 katika kuunga mkono nia thabiti hizo, kuimarisha uelewa wake, uthibitishaji, uhamasishaji wa utekelezaji wa sera ya nia thabiti ya usawa na haki kwa jamii;
- Dhana yetu kuhusu usawa na haki kwa jamii katika afya, yenye lengo la kukabili tofauti zisizo za haki katika afya na katika kupata huduma ya afya kupitia ugawaji upya wa rasilimali za jamii kwa afya, ikiwemo uwezo wa kudai, na uwezo wa kutumia rasilimali hizi;
- Upanuzi wa majimbo tunaojenga kwa ajili ya usawa na haki ya kijamii katika afya miongoni mwa serikali, wabunge, mabingwa wa afya, vyama vya wafanyaakzi na vyombo vingine vya vyama vya wanachi; watafiti na jamii katika ngazi ya kitaifa na kikanda;
- Changamoto zilizoletwa na mabadiliko mapya ya utandawazi kwa maadili yetu ya usawa na haki kwa jamii, kwa uwezo wa serikali na unyumbufu wa kutekeleza sera za serikali tunazochagua na kwa sekta ya afya ya umma na huduma muhimu ambazo ni za lazima kwa afya yetu;

### Mkutano wa EQUINET wa Juni 2004 uliofanyika Durban, Afrika Kusini, uliazimia kuwa tunatetea:

- Usawa na haki ya jamii katika afya;
- Maslahi ya umma dhidi ya biashara katika Afya;
- Uhusiano wa kimataifa na dunia unaokuza usawa, haki ya kijamii, afya ya wananchi na maslahi ya umma;
- Kuongezeka kwa mtiririko wa rasilimali usio na masharti kutoka Nchi zilizoendelea na masharti ya biashara yaliyo nafuu zaidi.

## MKUTANO WA TATU WA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU USAWA KATIKA AFYA, JUNI, 2004, MAAZIMIO

*Yanaendelea*

- Upunguzaji na pale inapowezekana urejeshaji wa rasilimali kutoka Nchi zinazoendelea kwenda Nchi zilizoendelea;
- Dhana ya haki za binadamu zinazohakikisha umuhimu wa jamii katika kudai stahiki za kijamii na kiuchumi, ubora wa vikundi vilivyo hatarini na vyenye mila na desturi za kiafrika za ujamaa;
- Mifumo ya usawa katika afya inayotoa huduma ya afya kwa wote, na ugawaji upya na kuelekeza rasilimali kwa wenye shida zaidi;
- Kuongeza uwekezaji katika afya kitaifa na kwenye sekta ya umma;
- Mifumo ya (huduma) afya inayokuza mikakati ya pamoja inayozingatia idadi ya watu kwa ajili ya afya na mpango mpana wa huduma ya afya ya msingi,
- Sera za biashara na kilimo zinazohakikisha utawala na usalama wa chakula kwa kaya kupitia ugawaji upya wa ardhi na uwekezaji katika wakulima wadogo wadogo kwa njia zinazokuza usawa wa jinsia na uzalishaji endelevu wa chakula;
- Angalau 15% ya bajeti ya Serikali iliyowekezwa katika sekta ya afya ya umma, kama ilivyoahidiwa Abuja, pamoja na kufutiwa madeni;
- Ugharimiaji wa mifumo ya afya unaozingatia uongezekaji wa kodi;
- Ugharimiaji wa afya usio na upendeleo, ambapo matajiri watachangia hisa kubwa ya mapato yao kwa afya kuliko maskini, pamoja na ruzuku mtambuko zilizoimarishwa kwa ajili ya mfuko wa mshikamano na hatari;
- Usawa, uwiano na upataji kwa bei nafuu dawa za kijenasi, na kutumia sera za dawa muhimu kwa watoa huduma ya afya wote;
- Sera za wafanyakazi zilizo sawa, zenye uwiano na za uadilifu katika ngazi ya taifa, kikanda na kimataifa, zikisaidiwa na fidia kwa ruzuku zilizopungua nchi za kusini-kaskazini zilizogharimiwa kupitia uhamaji wa wafanyakazi wa afya;
- Afya ya umma iliyo sawa na mwitikio shirikishi wa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa ajili ya ukuzaji wa kinga na afya, matibabu na huduma na kupunguza athari ya ugonjwa, hasa ndani na kwa ajili ya vijana na vikundi vilivyo hatarini;
- Upanuzi wa upataji wa dawa za kuongeza kinga kwa watu wanaoishi na UKIMWI katika nchi za Kusini mwa Afrika kama kipaumbele cha haraka, kwa kugharimia na mikabala inayoimarisha, na ambayo haiingiliani na mifumo na huduma zetu za afya ya umma;
- Nchi za kidemokrasia na zinazowajibika, zenye mamlaka kamili ya kutekeleza hatua za sera zilizo muhimu katika kulinda afya ya watu;
- Taratibu wakilishi na shirikishi zinazofaa na zenye nguvu kwa ngazi zote za sekta zetu za kijamii na afya na katika nchi kwa ujumla zaidi;
- Taratibu zinazofaa na zinazowajibika kwa ajili ya mchango wa umma na wa wadau kwa utoaji uamuzi katika afya;
- Mfungamano na ushirikiano ndani ya Afrika kuimarisha nchi za kidemokrasia, kuendeleza afya ya watu na kupambana na kutokutumia haki katika afya;
- Uongozi unaozingatia maadili kwenye mashirika yanayofanyakazi ya kukuza usawa katika afya.

Mkutano uliweka Mpango wa kazi na utekelezaji kwa EQUINET na wabia wake kwa ajili ya kutekeleza malengo haya.

*Kwa taarifa zaidi wasiliana na Sekretarieti ya EQUINET kupitia TARSC, admin@equinetafrica.org au angalia www.equinetafrica.org.*